# NOA BONGO JENGA MAISHA YAKO - MASWALA YA JAMII

**Kipindi cha sita: ‘ Sheria za Mchezo**"

**Mwandishi**: Chrispin Mwakideu

**Mhariri**: Andrea Schmidt

**WAHUSIKA**: Mapito(40),Roni(14),Eveline(19),Beti(12),kikosi cha wavulana(14+),kikundi cha waimbaji(12+),mkufunzi(35)

**Msimulizi**:

Hujambo na karibu tena katika kipindi hiki cha Noa Bongo Jenga Maisha Yako kuhusu vipi vijana wanavyoweza kushiriki katika siasa. Katika kipindi kilichopita tuliona jinsi vyombo vya habari vilivyo na jukumu muhimu katika kampeni ya Eveline kutaka kugombea kiti cha udiwani. Katika timu ya kandanda, Samu anavuliwa unahodha na kupewa Roni na Beti naye bado anakabiliwa na changamoto ya kuiunganisha kwaya yake. Karibu katika kipindi cha leo - ´´Sheria za Mchezo.

**Onyesho la kwanza: uwanja wa mpira**

**SFX: KIPENGA KINALIA**

**1.MKUFUNZI**: Wavulana.. hebu tuekeni duara.. leo kuna mgeni mashuhuri ambaye tunataka ajitambulishe, kisha baadaye aseme machache…hebu tumkaribisheni kama ilivyo desturi yetu.

**2.VIJANA**:(**WANAMSHANGILIA MAPITO KWA MAKOFI**)

Wuuuu!! Heko!!!!!!

**3.MAPITO:** Asanteni! Sikumbuki ni lini niliposhangiliwa namna hii…. Ni kitambo sana… asanteni! naitwa sajini Mapito.. Bila shaka kutokana na jina langu munaweza kutambua kwamba mimi ni babake Roni…

**4.VIJANA**: (**Shangwe zaidi**) Heeeee!!!! Wuuu!!!

**5.MAPITO**: Mimi ni afisa wa polisi.. na kazi yangu ni kuhakikisha kuna sheria na utengamano.. Sarti mutambue kwamba sheria zipo kwa ajili yenu wenyewe. Bila sheria hatuna tofuti yoyote na wanyama….

**6.VIJANA**: (**WANACHEKA**) HAHAHAHA……

**7.MAPITO**: Ni kweli. Familia, jamii au nchi yoyote ile lazima iwe na sheria za kuwaongoza watu wake. Hii haina maana kwamba kila mtu atazitii sheria hizi, lakini zinapovunjwa ni kazi yangu kuwakamata na kuwafungulia mashitaka watu wa aina hiyo kwa mujibu wa sheria.

**8.VIJANA**: Bwana Mapito, Samu jana alimsukuma Roni hapahapa kabla ya mazoezi. Anafaa akamatwe!

**9.MAPITO:**( **kwa kumaanisha**) Alifanyaje? Roni mbona hukunieleza kuhusu kisa hicho? Lakini hata hivyo, Samu hawezi kukamatwa kwa mujibu wa sheria kwa sababu yungali mdogo. Hii ina maana sheria inamchukulia bado ni mtoto na wala hajakuwa mtu mzima.

**10.VIJANA**: Ndio maana mkufunzi wetu alimtoa katika timu yetu…

**11.MAPITO:** Haha..(**acheka**) hata hivyo bado angali mdogo…

**12.VIJANA**: Alaaa! Kwa hiyo ina maana ninaweza kuiba sokoni na nisikamatwe? Je hiyo ndio maana ya kuwa juu ya sheria?

**13.MAPITO**: Hakuna aliye juu ya sheria.. hata mimi pia nikivunja sheria, nitahukumiwa.. Usijaribu uhalifu huo kwani utakaposhikwa.. na nakuhakikishia watakushika.. utaadhibiwa kwa kupelekwa shule ya kubadili tabia.. na niamini….huko hakuna raha kamwe…

**14.RONI**: Baba, ni nani anayeunda hizi sheria?

**15. MAPITO**: Roni nikiwa hapa kwa niaba ya mkufunzi niko kazini kwa hivyo niite sajini Mapito sio baba, hata hivyo ni swali zuri..wabunge pamoja na rais wanaochaguliwa na wananchi wakati wa uchaguzi mkuu ndiyo hutengeza sheria. Wajumbe hutunga mswada nakuupeleka bungeni kujadiliwa. Unapopitishwa hupelekwa kwa rais ambaye huutia sahihi mswada huo na kuufanya kuwa sheria.

**16.RONI**: Baba..oh! Samahani! sajini Mapito, inakuwaje wakati wabunge wanashindwa kukubaliana kuhusu mswada huo?

**17.WAVULANA**: ( **WAMCHEKA RON**I) Hehehe..

**18.MAPITO**: Wakishindwa kukubaliana mswada huwekwa kando, lakini mbunge yeyote yuko huru kuuleta tena bungeni wakati mwingine

**19.MKUFUNZI**: Kuna mwingine mwenye swali? Hapana.. Ok sawa, nimemualika sajini Mapito azungumze nasi kuhusu sheria na kwa nini tunazihitaji kwa sababu kama mjuavyo mchuano wa fainali unakaribia. Naa.. katika kabumbu pia kuna sheria za

mchezo, ukizivunja utaadhibiwa.

**20.KIJANA**: Mkufunzi, wakati mwingine marefa hutuadhibu kw amakosa madogo au? Kwa mfano kwenye mechi iliyopita, wanafanya hivyo kuzipendelea timu nyengine. Baadaye tuligundua kwamba mpwa wa refa alikuwa katika timu ile nyengine.

**21.MAPITO**: Ni kweli hayo hutokea na inasikitisha, lakini hata hivyo makosa hayo hayapaswi kutuzuia kutii sheria. Ushindi huwa mtamu wakati mtu anaposhinda kwa njia ya halali.

**22.MKUFUNZI**: Vijana, sajini Mapito anahitaji kuondoka sasa. Asante sana bwana Mapito kwa somo hilo na natumai nyinyi vijana mtafuata sheria.

**23.MAPITO**: Asanteni kwa kunialika na nawatakia kila la heri katika mchuano huo wa fainali…

**24.MKUFUNZI**; Hayo tosha kwa leo.. nataka mupumzike kabla ya pambano la fainali na mjiepushe na matatizo. Sitaki majeraha kabla ya mechi hiyo. Hip hip! Hip Hip!

**25.VIJANA**: Hureeee!

**26.MSIMULIZI**: Kipenga kimelia.. mafunzo yameingia barabara katika bongo za wachezaji wa kikosi cha Roni..Kwa upande mwingine Beti naye bado anapigana mieleka na kikundi chake cha waimbaji kilichogawanyika katika uwanja wa mashindano!

**<u>Onyesho la pili: katika ukumbi wa mashindano</u>**

**Muziki mororo**

**1.Mkuu wa sakafu: ( kupitia kipaza sauti)** Karibuni katika

mashindano ya muziki ya shule za msingi. Baada ya muda wa mapumziko, kwaya ya shule ya Milimani na kiongozi wao Betty Mapito itatuimbia wimbo wa Malaika…

**(Nje ya ukumbi)**

**2.BINTI**: Beti, mimi na kikundi changu tumeamuwa hatupandi jukwaani. Tunataka kuimba wimbo wetu wenyewe peke yetu.

**3.BETI**: Tafadhali nisikilize! Nilipoianzisha kwaya hii, sikuwa na lengo la kuanzisha mashindano ya umaarufu kati yako na mimi. Sheria za mashindano haya ziko wazi, kwaya sharti iwe na waimbaji zaidi ya kumi na unajua hakuna katiy etu aliye na watu kumi. Kwa hiyo tuchukulie huu ni wakati wa uchaguzi. Kama ujuavyo wakati wa uchaguzi watu hukosana lakini baadaye huungana kwa masilahi ya raia. Tuungane sasa kwa ajili ya shule yetu.

**4.BINTI**; Hmm.. Sijui. Unajua nikikubali kuungana na wewe, itakuwa ni kama umenishinda.

**5.BETI**: La, hapa sote tunashinda tunapoungana na kisha kujitahidi kuwashinda wapinzani wetu ambao ni kwaya nyengine.

**6.BINTI**: Nimependa wazo lako.. Vyema, basi tumekuwa marafiki. Kuanzia sasa mimi na kundi langu tuko pamoja na wewe.

**7.BET**I; (**kwa furaha**) Sawa twende nyuma ya jukwaa tusichelewe…

**8.BINTI:** Bado kuna shida moja zaidi…

**9.BETI**: Shida gani tena?

**10.BINTI**: Sijui nyie wenzangu lakini mimi nahisi uoga umeniingia.. tumbo langu ni kama limejaa vipepeo. Sijawahi kuimba mbele za watu…

**11.BETI**: Najau. Mimi mwenyewe pia naogopa. Lakini tuchukulie hamna mtu peyote ukumbini na sote tufurahie.! Sawa?

**12.Mkuu wa sakafu**: Tafadhali kila mtu aingie ukumbini sasa. Kwaya ya Milimani.. jukwaa ni lenu…

**13.BINT**I: Haiya ni sisi Beti..Oh hapana!

**14.MSIMULIZI**: Msikilizaji najua unashangaa na kujiuliza, waimbaji hawa watashinda kweli? Hayo ni baadaye lakini nyumbani kwa Mapito, Eveline amekasirika kweli kweli…

**<u>Onyesho la tatu: nyumbani kwa Mapito</u>**

**1.EVELINE**: (**hamaki**) Hapana baba si haki kamwe! Si haki!

**2.MAPITO**:(**amemakinika**) Si wewe peke yako Eve. Humfanyia hivyo kila mwanasiasa mpya.

**3.EVELINE**: Kwa nini waniharibie mabango yangu? Tuliyabandika jana tu na leo hayaonekani. Yale yaliyobakia yamevurugwa na kuharibiwa …Masikio yangu wameyachora marefu kwenye picha zangu hata punda afadhali…

**4.MAPITO**:( **akitulia** ) haya si mashindano ya urembo waache wachore masikio hata pua…huu ni uchaguzi…ukitaka kuwa mwanasiasa lazima uwe na ukakamavu. Ngoma hizo zalia, cheza msichana wangu. Furahi!

**5.EVELINE**: Baba, naweza kupeleka wapi malalamiko yangu?

Mbando hayo yalitugharimu pesa nyingi sana. Kwa nini watu wasishandane kwa haki badala ya kunifanyia unyama huu? Mimi siwezi kumuharibia mtu hata kama nina hakika ya kutomshinda…

**6.MAPITO:** Nilikutahadharisha kwamba haingekuwa rahisi. Ni vigumu sana kuwatia mbaroni watu hawa lakini nadhani unaweza kuwashtaki kwa tume ya uchaguzi lakini hakuna watakalofanya… huo ni mchezo wa siasa…

**7.BETI**: Baba tusirudi huko kwa sasa. Hata hivyo nitawapa habari kwani wao ndio wasimamizi wa uchaguzi… kesho asubuhi nitawatembelea.

**8.MAPITO**: Eveline nasikitika.. hii siasa huenda ikakushinda..

**9.EVELINE**: Baba mimi nataka kuleta mabidiliko…nikichaguliwa nitahakikisha vijana wasomi wanapata ajira zilizochukuliwa na watu wasio na vyeti eti kwa sababu ya kujuana.. wakulima wanaolipwa malipo duni watapa haki yao..haya ndio mabadiliko niliyoyalenga…na huo ni mwanzo tu

**10.MAPITO**: Eti mwanzo?mwanzo wa nini sasa?

**11.EVELINE**:  Baba , hii ni karne ya ishirini na moja.. iwapo sisi vijana hatutajitoa muhanga na kujihusisha na siasa za nchi siku zote tutabaki na lawama katika nchi hii.

**12.MAPITO:** Sijui nisemeje, lakini ujue mimi nina wasiwasi kama mzazi.

**13.EVELINE**: Kwa hivyo umenisamehe?

**14.MAPITO**: Nilikuamini lakini ukanivunja moyo…

**15.EVELINE**: Nielewe baba sio kupenda kwangu…

**16.MAPITO**: Iwe hivyo..Mbona Roni na Beti hawajarudi leo?

**17.EVELINE**: Beti alienda mashindanoni lakini Roni sifahamu aliko…

**28.MAPITO**: Nilikwenda kwenye mazoezi ya Roni leo lakini nimesahau kabisa kuhusu mashindano ya muziki ya akina Beti..

**MWISHO WA KIPINDI CHA SITA**

**Msimulizi:**
Ninahakika msikilizaji una dukuduku kuhusu yaliyotokea katika mashindano ya uimbaji. Basi ukitaka kuyajua hayo pamoja na yale yatakayotokea katika tume ya uchaguzi wakati Eveline atakapopeleka hoja zake na pia ukitaka kumshangilia Roni katika mchuano wa fainali, jiunge nasi juma lijalo. Unaweza kukisikiliza tena kipindi hiki kwenye tovuti yetu: www.dw-world.de/lbe Hadi wiki ijayo, kwaheri!